OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA
MITAA HALMASHAURI YA MANISPAA TABORA

Namba za simu:

Mkuu wa Shule 0785980771
Makamu Mkuu wa Shule 0787403900
Patron 0625995725

SHULE YA SEKONDARI MILAMBO
S.L.P 356,
TABORA.

TAREHE: ……..

Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi.
…….
S.L.P. ……
…….

YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MILAMBO
HALMASHAURI YA MANISPAA TABORA
MK0A TABORA MWAKA 2018/2019

1. Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha tano katika shule hii mwaka 2018/2019 tahasusi ya ……. Shule ya Sekondari Milambo ipo umbali wa kilomita moja magharibi mwa mji wa Tabora usafiri wa Taxi/Pikipiki/Bajaji unapatikana katika kituo cha mabasi mjini Tabora nauli ni Tshs. Taxi Tshs. 3000/=, Pikipiki 1000/= na Bajaji 2000/=.

2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-

2.1 Sare ya Shule

(a) Sare ya Shule hii ni Suruali mbili (2) light blue/summer blue za kitambaa na Mashati mawili (2) meupe ya mikono mirefu.
(b) Sare ya michezo kwa shule hii ni jezi ya nyekundu na bukta ya nyekundu.
(c) Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi.
(d) Soksi josi mbili nyeupe.
(e) Mkanda wa kuvalia suruali ni mweusi wa ngozi.(Mkanda wa begi hauruhusiwi
(f) Njoo na kiasi cha sh Tshs 13000/=kwa ajili ya sweta **(majaketi na aina nyingine ya nguo haviruhusiwi)**
(g) Tai rangi ya blue mpauko (Light blue) mbili au uje na Tshs. 5000/=
(h) Njoo na Tsh. 28000 /= kwa ajili ya tisheti mbili(2) .

2.2 Ada na michango ya Shule:

(a) Ada ya shule kwa mwaka ni Tshs. 70,000/=. Unaweza kulipa Shilingi 35,000/= kwa muhula au kulipa ada yote kwa mara moja. Fedha hizo zilipwe kwenye Akaunti ya Shule Na. **51001100069** katika Benk ya NMB (***tafadhali andika jina la mwanafunzi pay in slip na sio jina la mzazi).***

(b) Michango inayotakiwa kulipwa na kila mzazi ni:-

i. Shilingi 15,000/= kwa ajili ya ukarabati wa samani
ii. Shilingi 8,000/= kwaajili ya kitambulisho, picha na Kamba/ beji ya shingoni
iii. Shilingi 20,000/= kwa ajili ya Taaluma
iv. Shilingi 30,000/= kwa ajili ya kuwalipa wapishi, walinzi na vibarua wengine.
v. Shilingi 2,000/= kwa ajili ya nembo ya shule kwa shati moja.
vi. Shilingi 10,000/= kwa ajili ya huduma ya kwanza.
vii. Shilingi 20,000/= Mitihani ya kujipima mock kanda.
viii. Fedha ya tahadhari 5,000/= (haitalejeshwa).
ix. Shilingi 15,000/= kwa ajili ya mock mkoa

MICHANGO MINGINE WEKA KWENYE AKAUNTI NA. 51001100132 NMB

Angalizo Jumla ya ada na michango kwa wanafunzi ni Shilingi Tsh.**193,000/=**

C. Mahitaji muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuleta shuleni ni:-

i. Ream moja ya karatasi za kudurufu nyeupe (A4) (kwa mwaka) au aje na Tshs. 10,000/=
ii. Vitabu vya tahasusi husika kulingana na mchepuo wake
iii. Dissecting kit kwa wanafunzi wa Biolojia
iv. Scientific calculator(kikokotozi) kwa wanafunzi wa hesabu na sayansi
v. Godoro 2.5 x 6 ft au njoo na Tshs 45000/=
vi. Mashuka pair 2 rangi right blue (au aje na Tsh 16000/=), blanketi 1, foronya 1, chandurua 1
vii. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli,kijiko na kikombe visiwe vya plastiki.
viii. Ndoo mbili ndogo zenye mifuniko.
ix. Fyekeo moja, mfagio wa ndani (soft bloom) mfagio wa nje (CHELEWA YENYE MTI) water squeezer na jembe yenye mpini.
x. Sanduku la bati (trunk) kwa ajili ya kutunzia vifaa vyake vikiwemo vitabu na madaftari
xi. Mwanafunzi harusiwi kuja na nguo za nyumbani maana atakuwa anashindia sare za shule(shati, t-shet na suruali nyeusi) aidha mwanafunzi ajapo shuleni aje amevaa sare ya shule (suruali nyeusi ya kitambaa isiwe ya kubana mwili au mtepesho na shati nyeupe.

NB. Michango ya tai, sweta,kitabulisho na picha,muhuri, rimu, godoro na tisheti njoo na hela mkononi . vitu vifuatavyo vinapatikana shuleni, suluari 20,000/= shati 8000/= madaftari na scientific calculator vinapatikana kwenye duka la shule.

KANUNI NA SHERIA ZA SHULE

Kila mwanafunzi anatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ili kuleta ufanisi mzuri wa taasisi pamoja na matarajio mazuri yako mwenyewe.

A). SHERIA NA KANUNI ZA SHULE HII.

i). Heshima kwa uongozi, wazazi na wafanyakazi kwa ujumla.

ii). Mahudhurio mazuri katika kila shughuli zifanyikazo ndani na nje ya shule.

iii). Kuwahi katika shughuli za shule utakazopewa.

iv). Kufahamu na kuheshimu mipaka ya shule.

v). Kutotoka nje ya shule bila sare ya shule na ruhusa ya maandishi.

vi). Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule kwa ujumla.

vii). Kuvaa sare ya shule wakati wote unaotakiwa.

viii). Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote. Ni marufuku kuwa bwenini wakati wa shughuli za darasani.

ix). Kuheshimu na kusimama wima bendera ya Taifa inapopandishwa na wimbo wa Taifa unapoimbwa.

x). Kuishi maisha ya ushirikiano na upendo na wenzako.

xi) Kutotoa matusi na lugha chafu, kuzomea au kuanzisha fujo au kushiriki katika migomo.

xii). Kusalimia wafanyakazi au mtu yeyote anayestahili anapopita ndani au nje ya darasa.

xiii). Kutomiliki kifaa chochote cha umeme kama pasi , chaja, simu nk.

xiv). Kulipa michango yote ya shule kwa wakati ili kuepuka usumbufu.

xv). Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni .

xvi). Kufanya mitihani yote ya ndani na nje.

xvii). Kuvaa kitambulisho cha shule wakati wote ndani na nje ya shule

B). MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE

i. Wizi
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku tisini (90) bila taarifa/ utoro
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi mwenzake , mwalimu,/ mlezi na jamii kwa ujumla
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyeto yule
vi. Ulevi au unywaji wa wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya
vii. Uvutaji wa sigara
viii. Uasherati uhusiano wa jinsia moja au kuoa au kuolewa
ix. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi.
x. Kusababisha mimba au kumpa mimba msichana
xi. Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni
xii. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule.
xiii. Kudharau bendela ya taifa
xiv. Kufanya jaribio lolote la kujiua kama kunywa sumu n.k
xv. Uhalibifu wa mali ya ummaa kwa makusudi

C. MKATABA WA KUFUATA TARATIBU NA SHERIA ZA SHULE

Mimi (Jina la mwanafunzi)…… Kidato cha……Tahasusi……
Nimesoma na kuelewa sheria, kanuni na taratibu zote za shule hii, na niko tayari kuzitekeleza kwa muda wote nitakapokuwa shuleni hapa kama mwanafunzi. Nitakapo kiuka kipengele chochote cha shule adhabu stahili ichukuliwe dhidi yangu kwa mujibu wa sheria na taratibu.

……. …….
Saini ya Mwanafunzi **Mkuu wa Shule**

4. VIAMBATANISHO NA FOMU MUHIMU

a. Fomu ya uchunguzi wa afya (medical examination form) ambazo zinajazwa na mganga mkuu wa hospitali ya serikali
b. Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi/ mkataba wa kutoshiriki katika mgomo ,fujo na makosa ya jinai
c. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria na kanuni, kulipa ada, michango ya maelekezo mengine yatakayotolewa na shule
d. Picha nne(4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pampja na namba zao za simu.

Nb . tafadhari soma kwa makini maelekezo/ maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

Karibu sana katika shule ya milambo

Saini ya mkuu wa shule ……

Jina la mkuu wa shule ……

Mhuri wa mkuu wa shule……..

FOMU YA MZAZI KUKIRI KUKUBALIANA NA SHERIA, KANUNI NA MAELEKEZO MENGINE YATAKAYOTOLEWA NA SHULE

Mimi……Mzazi/ Mlezi wa Mwanafunzi…….
….

Nimesoma na kuzielewa sheria, kanuni na taratibu za shule na nimekubaliana nazo kama mzazi/ mlezi wa mwanafunzi na niko tayari kuzitekeleza sheria hizo pamoja na maelezo mengine yatakayotolewa na shule.

……

Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi

NB: ***KUTAKUWA NA KIKAO CHA WAZAZI WOTE TAREHE 28.09.2018(IJUMAA). FIKA BILA KUKOSA ILI TUJADILIANE KWA PAMOJA, PIA KUFAHAMU MWENENDO WA WATOTO KITAALUMA NA KINIDHAMU.***

SHULE YA SEKONDARI MILAMBO

A. FOMU YA MAELEKEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI

1. Jina kamili la Mwanafunzi…….…….
2. Tarehe ya kuzaliwa…….……..….
3. Mzazi/ Mlezi…….……..
4. Uhusiano na Mlezi……..
5. Mahali anapoishi Mzazi/Mlezi, Mkoa…….……
   Wilaya ya……Mtaa/Kijiji……..……..
6. Mawasiliano ya Mzazi/Mlezi…….……..
7. Kabila…….….Dini……..…….
8. Kazi ya Mzazi/Mlezi……..…….
9. Wazazi wako hai au wamefariki (weka alama ya √)

   - Baba (amefariki) ( ) Baba yupo hai ( )
   - Mama (amefariki) ( ) Mama yupo hai ( )

10. Ndugu wengine wa karibu na Mzazi/Mlezi ambao wanaweza kutumika kama walezi wa mwanafunzi kama mzazi/mlezi husika hayupo.

a. ……..……. Mahali ……..
b. ……..……. Mahali ……..
c. ……..……. Mahali ……..
d. ……..……. Mahali ……..

11. **SANDUKU LA POSTA LA MZAZI/MLEZI KWA AJILI YA KUTUMA MATOKEO:-**
    ……
    ……
    ……..

B. MKATABA WA KUTOSHIRIKI KATIKA MGOMO, FUJO NA MAKOSA YA JINAI

Mimi (Jina la mwanafunzi)…….
Nimesoma na kuelewa sheria, kanuni na taratibu zote za shule ya bweni, na niko tayari kuzitekeleza kwa muda wote nitakapokuwa shuleni hapa kama mwanafunzi. Nitakapo kiuka kipengele chochote cha shule hivyo adhabu stahili ichukuliwe dhidi yangu kwa mujibu wa sheria na taratibu.

……. …….
Saini ya Mwanafunzi **Mkuu wa Shule**

MEDICAL EXAMINATION FORM

Medical examination form to completed by government medical officer and return to the Head master Milambo secondary school

Student full name……
.
Present age……..

Blood test…….……..…….

Examination stool……

T.B test……..

Asthma…….……

Eye disorder……

Nose disorder……..

Ear disorder ……..

Skin disease……
Anemia……

Chest……..……

Operations…….…….
Serious Accidents……..……

Any other infections disease……..……
Pregnancy……..…….
Additional information e.g. Physical defects or impairment, chronic or family diseases etc…….……...
……
……

I certify that I have personally examined Mr./Miss……and found him/her fit unit to purpose studies

Signature…….

Designation…….

(Official rubber stamp) ……..